

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA MMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJISAFI NA MAJITAKA KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA NJOMBE (NJOMBE WSSA) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

Mnamo tarehe 18 Machi 2019, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Njombe (Njombe WSSA). Njombe WSSA wanaomba mabadiliko ya bei kwa huduma za majisafi kwa kipindi cha 2019/20 - 2021/22. Majedwali namba 1 - 5 yanaonesha mchanganuo wa bei na ada za sasa zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majisafi kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/Uniti)

Kundi la Wateja	Matumi zi kwa Uniti	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
			2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21	Mabadiliko kwa asilimia
Majumbani	0-5	900	63%	1,469	63%	2,398	15%	2,749
	6-10	980	63%	1,600	63%	2,611	15%	2,994
	>11	1,000	63%	1,632	63%	2,665	15%	3,055
Taasisi	1-5	1,000	63%	1,632	63%	2,665	15%	3,055
	6-10	1,100	63%	1,796	63%	2,931	15%	3,360
	>10	1,150	63%	1,877	63%	3,064	15%	3,513
Biashara	1-5	1,000	63%	1,632	63%	2,665	15%	3,055
	>5	1,100	63%	1,796	63%	2,931	15%	3,360
Viwanda	1 - 5	1,000	63%	1,632	63%	2,665	15%	3,055
	>5	1,100	63%	1,796	63%	2,931	15%	3,360
Magati		1,000	50%	1,500	0%	1,500	0%	1,500

Jedwali 2: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majisafi kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa
-----------------	-------------	----------------------

	2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	13,650	55%	21,221	30%	27,634	-	Hakuna

Jedwali 3: Tozo ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Iliyopendekezwa
	Mpaka tarehe 31 Machi 2019	Kuanzia tarehe 1 Aprili 2019
Majumbani	3000	Hakuna tozo
Taasisi	4000	
Biashara	4000	
Viwanda	4000	

Jedwali 4: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kuunganishiwa Huduma ya Majisafi (TZS/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Inayopendekezwa
	2018/19	2019/20 – 2021/22
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za vifaa vya maunganisho na nguvu kazi kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 24 cha Kanuni za Majisafi za mwaka 2013	Asilimia 20 ya gharama za vifaa vya maunganisho na nguvu kazi kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 24 cha Kanuni za Majisafi za mwaka 2013
Taasisi		
Biashara		
Viwanda		

Jedwali 5: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	20,000	25%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Taasisi	25,000	20%	30,000	0%	30,000	0%	30,000
Biashara	25,000	20%	30,000	0%	30,000	0%	30,000
Viwanda	25,000	20%	30,000	0%	30,000	0%	30,000

Sababu kuu zilizopelekea kuomba mabadiliko ya bei kama ilivyoelezwa na Njombe WSSA ni: kutakiwa kuanza kujitegemea kikamilifu katika uendeshaji ikiimanisha hakuna fedha itakayotolewa kusaidia uendeshaji wa Mamlaka. Pia Njombe WSSA imeelza kuwa gharama nyingi za uendeshaji kama vile bei za vifaa na madawa zimeongezeka tangu mapitio ya mwisho ya bei.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 2 Mei 2019 kwenye ukumbi wa Turbo uliopo mjini Njombe** kuanzia saa **3:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Njombe WSSA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 6 Mei 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika **OFISI ZA EWURA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI, GHOROFA YA SITA, JENGO LA NHIF – MTAA WA KARUME** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ZILIZOPO MJI WA NJOMBE**.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)